TANGAZO LA SERIKALI Na. 503 la tarehe 21/7/2023

SHERIA YA PETROLI
(SURA 392)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha128(3)*)

TANGAZO LA KIBALI CHA UJENZI WA KITUO CHA GESI ASILIA KWA KAMPUNI YA TAQA DALBIT KATIKA ENEO LA BARABARA YA SAM NUJOMA, 2023

Jina

1. Tangazo hili litajulikana kama Tangazo la Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Gesi Asilia kwa Kampuni ya TAQA Dalbit katika Eneo la Barabara ya Sam Nujoma, 2023.

Tafsiri

2. Katika Notisi hii, isipokuwa kama mukhtadha unahitaji vinginevyo:

"mwombaji" maana yake ni kampuni ya TAQA Dalbit wa S.L.P. 76908 Dar es Salaam;

Sura. 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji; na

Sura 392

"Kibali cha Ujenzi" maana yake ni kibali kilichotolewa na Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 128(1) cha Sheria ya Petroli.

Kutolewa kwa Kibali cha Ujenzi

3. Kibali cha Ujenzi kimetolewa kwa mwombaji kujenga kituo cha kujaza gesi asilia katika Kiwanja Na. 2005/5/1/3, Kitalu C, Ubungo kilichopo eneo la barabara ya Sam Nujoma, Dar es Salaam kwa vigezo na masharti yafuatayo:

(a) ujenzi hautaanza mpaka mwombaji awe amepata cheti cha tathmini ya athari za mazingira kutoka mamlaka husika;

(b) kuzingatia muundo ulioidhinishwa, vipimo

vya kiufundi, taratibu (ufungaji, ujenzi, uchomeleaji, majaribio na uendeshaji), mkuza na sheria nyingine zinazohusika;

(c) kuhakikisha kuwa kituo cha gesi asilia na vifaa vyake vinajengwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa au sheria husika;

(d) kuhakikisha kuwa ukaguzi wa ujenzi wa kituo na vifaa vyake wakati wa ujenzi unafanyika kadri inavyohitajika ili kuhakikisha kuwa ujenzi, vifaa, uchomeleaji, maunganisho na ujaribuji wa kituo baada ya kukamilika unafanyika kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa;

(e) kuhakikisha kuwa hakuna au kupunguza usumbufu kwa wakazi walio karibu na eneo la ujenzi na usalama kwa umma upewe kipaumbele. Endapo ulipuzi utafanyika, ufanywe kwa kuzingatia taratibu za kisheria zilizopo na kufanywa na mtu mwenye sifa za kazi ya ulipuzi kwa kuzingatia usalama kwa umma, mifugo, wanyama, majengo, miundombinu ya simu, umeme, miundombinu ya chini ya ardhi na mali nyingine zilizo karibu na eneo kunakofanyika ulipuzi;

(f) kuhakikisha kuwa zinakuwepo juhudi za kupunguza uharibifu kwenye ardhi na kuzuia mazingira yatakayosababisha kuziba kwa mifereji ya kupitisha maji na mmomonyoko wa udongo. Baada ya ujenzi, ardhi itapaswa kurudishwa katika hali iliyokuwepo kwa kadri itakavyowezekana;

(g) Kuzingatia viwango vya mazingira, afya na usalama vilivyoainishwa na sheria. Afya na usalama wa watu na vifaa vitapaswa kuzingatiwa na kuhakikisha matumizi ya vifaa vya usalama (PPE) wakati wote kama vile kofia ngumu, miwani na viatu vya

usalama na matumizi ya kizima moto; na

(h) Kuhakikisha kuwa miundombinu yote ya utoaji huduma kwa umma bila kujali kuwa inadhibitiwa na mamlaka au la inalindwa dhidi ya uharibifu na kuwaarifu wamiliki wake wawepo eneo la ujenzi wakati wa kujenga.

Ukomo wa Kibali cha Ujenzi

4. Kibali cha Ujenzi kitakoma endapo ujenzi hautaanza ndani ya miezi ishirini na nne tangu tarehe kilipotolewa.

Dodoma,
10 Julai, 2023

JAMES A. MWAINYEKULE,
*Mkurugenzi Mkuu*